JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

www.vpo.go.tz

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# UTARATIBU WA VIKAO VYA KAMATI YA PAMOJA YA SMT NA SMZ YA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA MUUNGANO

**Aprili, 2019**

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA MAKAMU WA RAIS

## UTARATIBU WA VIKAO VYA KAMATI YA PAMOJA YA SMT NA SMZ YA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA MUUNGANO

**Aprili, 2019**

# Yaliyomo


**DIBAJI......iii**

**1.0 UTANGULIZI......1**

**2.0 KIKAO CHA KAMATI YA PAMOJA YA SMT NA SMZ YA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA MUUNGANO .2**

2.1 Wajumbe......2

2.2 Majukumu......3

2.3 Uendeshaji wa Kikao cha Kamati ya Pamoja......3

**3.0 KIKAO CHA MAWAZIRI WA SMT NA SMZ......4**

3.1 Wajumbe......4

3.2 Majukumu......5

3.3 Uendeshaji wa Kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ......6

**4.0 KIKAO CHA MAKATIBU WAKUU WA SMT NA SMZ 6**

4.1 Wajumbe......6

4.2 Majukumu......7

4.3 Uendeshaji wa Kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ8

**5.0 VIKAO VYA KAMATI YA FEDHA, UCHUMI NA BIASHARA NA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA......8**

5.1 Wajumbe......9

**5.1.1 Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara ni:-......9**

**5.1.2 Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ni:-......10**

5.2 Majukumu ........................................................................ 11

5.3 Uendeshaji wa Vikao ........................................................ 11

**6.0 SEKRETARIETI YA KAMATI YA PAMOJA YA SMT NA SMZ YA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA MUUNGANO ........................................ 12**

6.1 Wajumbe .......................................................................... 12

6.2 Majukumu ......................................................................... 13

6.3 Uendeshaji wa Kikao ........................................................ 13

**7.0 VIKAO VYA SEKTA................................................ 13**

7.1 Wajumbe .......................................................................... 14

7.2 Uendeshaji wa Vikao vya Sekta ........................................ 14

7.3 Uwasilishaji wa Hoja ........................................................ 14

7.4 Uondoshwaji wa Hoja ....................................................... 14

7.5 Gharama za Vikao ............................................................ 15

**8.0 TATHMINI NA UFUATILIAJI .................................. 15**

**9.0 HITIMISHO.............................................................. 15**

# DIBAJI



Mhe. Samia Suluhu Hassan

Muungano huu umedumu kutokana na dhamira za dhati za umoja walizokuwa nazo Waasisi wake, Sera makini za Serikali zote mbili za TANU na ASP na sasa CCM, jitihada zinazoendelezwa na viongozi waliofuatia baada ya Waasisi pamoja na kuungwa mkono na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, mifumo imara iliyowekwa ya kujadili na kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoukabili Muungano wetu, imewezesha pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano kupiga hatua kubwa kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na hivyo kupata sifa kubwa kimataifa.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano iliyoundwa mwaka 2005 imekuwa ni nyenzo muhimu katika kuimarisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioasisiwa mwaka 1964. Vikao mbalimbali vinavyojumuisha wajumbe kutoka pande zote mbili za Muungano vimekuwa vikifanyika katika ngazi za Wataalam, Makatibu Wakuu, Mawaziri na Kamati ya Pamoja chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuhakikisha changamoto zote zinatafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utatuzi wa changamoto zilizojadiliwa na kupatiwa ufumbuzi tangu mwaka 2006, Serikali zetu mbili zimeandaa Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano ili kuongeza kasi ya uratibu wa vikao na ufuatiliaji wa maagizo, maelekezo na maamuzi yanayotolewa katika vikao hivyo.

Utaratibu huu, tulioupitisha kwenye Kikao cha Kamati ya Pamoja cha tarehe 9 Februari, 2019, unaimarisha na kurasimisha utaratibu wa vikao vya pamoja na kuweka muda kwa vikao vya kila ngazi. Uimara wa Muungano wetu hautokani na kukosekana kwa changamoto bali unatokana na kuwepo kwa mifumo thabiti na utashi wa kisiasa wa kuzishughulikia. Nina imani kwamba, Utaratibu huu utatekelezwa kwa ukamilifu.

Mwisho, nawashukuru viongozi na watendaji wa ngazi mbalimbali kutoka pande zote mbili za Muungano kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazoukabili Muungano wetu. Aidha, ninapenda kuwakumbusha watanzania wote kuwa, "**Tunalo jukumu la kuuenzi na kuuendeleza Muungano kwa faida yetu na kizazi kijacho**".

Mhe. Samia Suluhu Hassan

**MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## 1.0 UTANGULIZI

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliasisiwa tarehe 26 Aprili, 1964, tangu kuasisiwa kwake kumekuwa na mafanikio katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto katika kutekeleza mambo ya Muungano. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zimechukua hatua za kuhakikisha kuwa changamoto hizo zinapatiwa ufumbuzi. Hatua hizo ni pamoja na kuundwa kwa Tume na Kamati za kutatua changamoto hizo, kwa mfano Kamati ya Shellukindo ya mwaka 1992.

Mwaka 2005 Serikali iliendeleza jitihada hizo kwa kuanzisha vikao vya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jitihada hizo ziliendelea hadi mwezi Februari, 2008, ilipoundwa Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano (Kamati ya Pamoja).

Vikao vya Kamati ya Pamoja vitakuwa kwenye ngazi tatu ambazo ni:-

a. Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia masuala ya Muungano;
b. Kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ; na
c. Kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ.

Vikao vyote huratibiwa na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano.

## 2.0 KIKAO CHA KAMATI YA PAMOJA YA SMT NA SMZ YA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA MUUNGANO

Hiki ni kikao cha ngazi ya juu kabisa katika mtiririko wa vikao vya Kamati ya Pamoja.

### 2.1 Wajumbe

Kikao hiki kitahusisha wajumbe wafuatao: -

a. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mwenyekiti;
b. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mjumbe;
c. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar - Mjumbe;
d. Mawaziri wote – SMT - Wajumbe;
e. Mawaziri wote – SMZ - Wajumbe;
f. Mwanasheria Mkuu – SMT - Mjumbe;
g. Mwanasheria Mkuu – SMZ – Mjumbe;
h. Katibu Mkuu Kiongozi – SMT – Mjumbe;
i. Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi – SMZ – Mjumbe;
j. Makatibu Wakuu wote - SMT - Wajumbe;
k. Makatibu Wakuu wote – SMZ - Wajumbe;
l. Naibu Mwanasheria Mkuu – SMT - Mjumbe; na
m. Naibu Mwanasheria Mkuu – SMZ – Mjumbe.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira – SMT atakuwa Katibu wa kikao hiki akishirikiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja itashauri kumualika mjumbe mwingine itakavyoonekana inafaa.

Iwapo Waziri Mkuu au Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar atashindwa kuhudhuria kikao, atamjulisha Mwenyekiti. Endapo kikao hicho hakiwezi kuahirishwa, Waziri Mkuu/Makamu wa Pili wa Rais atateua Waziri mwandamizi kutoka Serikali husika kukaimu nafasi yake wakati wa kikao na Waziri huyo atakua na Mamlaka kamili ya nafasi aliyokaimishwa.

## 2.2 Majukumu

Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano, kitakuwa na majukumu yafuatayo: -

a. Kupokea taarifa za utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa katika Kikao cha Kamati ya Pamoja;
b. Kutoa uamuzi wa makubaliano yaliyofikiwa katika kikao cha Mawaziri;
c. Kutoa maelekezo na maagizo kwa hoja ambazo hazijapatiwa ufumbuzi;
d. Kuidhinisha hoja mpya na kuzitolea maelekezo; na
e. Kutoa maelekezo kwa masuala yoyote yatakayokua na maslahi katika Muungano.

## 2.3 Uendeshaji wa Kikao cha Kamati ya Pamoja

Kikao cha Kamati ya Pamoja kitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao: -

a. Kikao kitafanyika mara moja kwa mwaka na Mwenyekiti anaweza kuitisha kikao maalum itakapohitajika;

b. Uamuzi wa kikao utafanywa na Mwenyekiti baada ya kushauriwa na Waziri Mkuu wa SMT na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar au Waziri atakaepewa nafasi hiyo; na
c. Kikao kitafanyika pande zote mbili za Muungano kwa mzunguko. Hata hivyo, kinaweza kufanyika upande mmoja mfululizo kwa makubaliano.

## 3.0 KIKAO CHA MAWAZIRI WA SMT NA SMZ

Kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ kitakua kikao cha ngazi ya pili katika mtiririko wa vikao vya Kamati ya Pamoja.

Vikao hivi vitaongozwa na Mwenyekiti kwa kushirikiana na Mwenyekiti Mwenza. Kikao kikifanyika Tanzania Bara, Mwenyekiti wa kikao atatoka SMT na Mwenyekiti Mwenza atatoka SMZ au kinyume chake.

### 3.1 Wajumbe

Wajumbe wa kikao hiki watakuwa ni:-

a. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira–Mwenyekiti/ Mwenyekiti Mwenza
b. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais–Zanzibar-Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza
c. Mawaziri wote – SMT - Wajumbe;
d. Mawaziri wote – SMZ - Wajumbe;
e. Mwanasheria Mkuu – SMT - Mjumbe;
f. Mwanasheria Mkuu – SMZ - Mjumbe;
g. Katibu Mkuu Kiongozi wa SMT - Mjumbe;

h. Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi– SMZ - Mjumbe;
i. Makatibu Wakuu wote – SMT - Wajumbe;
j. Makatibu Wakuu wote – SMZ - Wajumbe;
k. Naibu Mwanasheria Mkuu – SMT - Mjumbe;
l. Naibu Mwanasheria Mkuu – SMZ - Mjumbe;
m. Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais – SMT - Katibu/ Katibu Mwenza; na
n. Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – SMZ - Katibu/Katibu Mwenza.

Sekretarieti inaweza kushauri kualikwa kwa washiriki wengine itakapoonekana inafaa.

### 3.2 Majukumu

Kikao hiki kitakuwa na majukumu yafuatayo:-

a. Kupokea taarifa za utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa katika kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ;
b. Kutoa uamuzi kwa makubaliano yaliyofikiwa katika kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ;
c. Kutoa maelekezo na maagizo kwa Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ juu ya hoja ambazo hazijapatiwa ufumbuzi;
d. Kutekeleza maagizo ya kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano;
e. Kutoa ushauri kwa Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano; na
f. Kupokea na kupitisha hoja mpya.

### 3.3 Uendeshaji wa Kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ

Kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ kitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao: -

a. Kikao kitafanyika mara moja kwa mwaka na kutokana na mahitaji kikao maalum kitaitishwa;
b. Uamuzi wa kufanya kikao utafanywa na Mwenyekiti baada ya makubaliano na Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais;
c. Kikao kitafanyika pande zote mbili za Muungano kwa mzunguko. Hata hivyo, kinaweza kufanyika upande mmoja mfululizo kwa makubaliano.

## 4.0 KIKAO CHA MAKATIBU WAKUU WA SMT NA SMZ

Kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ kitakua kikao cha ngazi ya tatu katika mtiririko wa vikao vya Kamati ya Pamoja.

Iwapo Mwenyekiti atapata dharura itakayosababisha kutoweza kuongoza kikao, atalazimika kufanya mawasiliano na Mwenyekiti Mwenza ili kikao kifanyike.

### 4.1 Wajumbe

Wajumbe wa kikao hiki ni:-

a. Katibu Mkuu Kiongozi wa SMT– Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza
b. Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi- Mwenyekiti / Mwenyekiti Mwenza;
c. Makatibu Wakuu wote – SMT – Wajumbe;

d. Makatibu Wakuu wote – SMZ - Wajumbe;
e. Naibu Mwanasheria Mkuu wa SMT - Mjumbe;
f. Naibu Mwanasheria Mkuu wa SMZ - Mjumbe;
g. Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais SMT - Katibu/ Katibu Mwenza; na
h. Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais SMZ - Katibu/Katibu Mwenza.

Sekretarieti inaweza kushauri kualikwa kwa washiriki wengine inapoonekana inafaa.

### 4.2 Majukumu

Kikao hiki kitakuwa na majukumu yafuatayo: -

a. Kutekeleza maagizo yaliyotolewa katika kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ na kuwasilisha taarifa;
b. Kupokea taarifa za utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa katika kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ;
c. Kutoa uamuzi wa makubaliano yaliyofikiwa katika vikao vya kisekta;
d. Kutoa maagizo kwa sekta husika za SMT na SMZ;
e. Kutoa ushauri kwa Mawaziri wa SMT na SMZ; na
f. Kupokea, kujadili na kuwasilisha hoja mpya katika kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ.

### 4.3 Uendeshaji wa Kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ

Kikao cha Makatibu wa Wakuu wa SMT na SMZ kitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao: -

a. Kikao kitafanyika mara mbili kwa mwaka, kutokana na mahitaji kikao maalum kinaweza kuitishwa;
b. Uamuzi wa kikao utafanywa na Mwenyekiti baada ya makubaliano ya Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ; na
c. Kikao kitafanyika pande zote mbili za Muungano kwa mzunguko. Hata hivyo, kinaweza kufanyika upande mmoja mfululizo kwa makubaliano.

## 5.0 VIKAO VYA KAMATI YA FEDHA, UCHUMI NA BIASHARA NA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA

Kutakuwa na Kamati mbili zitakazoundwa na wajumbe kutoka katika Kamati ya Pamoja. Kamati hizo ni Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kamati hizi zimeundwa kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazohitaji utatuzi wa haraka badala ya kusubiri utaratibu wa kawaida wa Vikao vya Kamati ya Pamoja vya SMT na SMZ. Kamati hizi zitawasilisha taarifa ya utekelezaji katika Vikao vya Kamati ya Pamoja vya SMT na SMZ. Aidha, vikao hivi vitaratibiwa na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano.

## 5.1 Wajumbe

### 5.1.1 Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara ni: -

a. Waziri wa Fedha na Mipango, SMT– Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza;
b. Waziri wa Fedha na Mipango, SMZ – Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza;
c. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, SMT – Mjumbe;
d. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar - Mjumbe;
e. Waziri wa Viwanda na Biashara, SMT - Mjumbe;
f. Waziri wa Biashara na Viwanda, SMZ - Mjumbe;
g. Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano – SMT – Mjumbe;
h. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, SMZ – Mjumbe;
i. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji, SMT – Mjumbe;
j. Makatibu Wakuu wa Viwanda na Biashara, SMT na SMZ - Wajumbe;
k. Makatibu Wakuu wa Fedha na Mipango, SMT na SMZ - Wajumbe;
l. Makatibu Wakuu wa Uchukuzi, SMT na SMZ – Wajumbe;
m. Gavana wa Benki Kuu wa Tanzania – Mjumbe;
n. Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, SMT – Katibu/ Katibu Mwenza; na
o. Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar – Katibu/Katibu Mwenza.

### 5.1.2 Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ni: -

a. Waziri wa Katiba na Sheria, SMT– Mwenyekiti / Mwenyekiti Mwenza;
b. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, SMZ– Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza;
c. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, SMT - Mjumbe;
d. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar - Mjumbe;
e. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, SMZ – Mjumbe;
f. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira na Ulemavu, SMT – Mjumbe;
g. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, SMT – Mjumbe;
h. Mwanasheria Mkuu, SMT – Mjumbe;
i. Mwanasheria Mkuu, SMZ – Mjumbe;
j. Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria, SMT – Mjumbe ;
k. Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, SMT – Mjumbe;
l. Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, SMZ – Mjumbe ;
m. Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, SMT – Katibu/ Katibu Mwenza; na
n. Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar – Katibu/Katibu Mwenza.

Mwenyekiti anaweza kumwalika mjumbe mwingine kadri itakavyoonekana inafaa.

### 5.2 Majukumu

Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara na Kamati ya Katiba, Sheria Utawala na zitakuwa na majukumu yafuatayo: -

a. Kujadili na kubuni mbinu za kutatua changamoto zinazohitaji ufumbuzi wa haraka kwa sekta husika;
b. Kutoa taarifa za utekelezaji wa changamoto zilizopatiwa ufumbuzi kwa Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ; na
c. Kuwasilisha taarifa ya hoja zinazohitaji maamuzi kwa Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ.

### 5.3 Uendeshaji wa Vikao

Vikao vya Kamati hizi mbili vitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao: -

a. Vikao vitafanyika muda wowote itakapotokeza haja ya kukutana;
b. Uamuzi wa vikao utafanywa na Mwenyekiti baada ya makubaliano ya Wajumbe; na
c. Vikao vitafanyika pande zote mbili za Muungano kwa kupokezana. Hata hivyo, vinaweza kufanyika upande mmoja mfululizo kwa makubaliano.

# 6.0 SEKRETARIETI YA KAMATI YA PAMOJA YA SMT NA SMZ YA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA MUUNGANO

## 6.1 Wajumbe

Kutakuwa na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano ambayo itaratibu ngazi zote za vikao vya Kamati ya Pamoja yenye wajumbe wafuatao: -

a. Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais – SMT – Mwenyekiti/ Mwenyekiti Mwenza;
b. Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – SMZ - Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza;
c. Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – SMT - Mjumbe;
d. Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria, SMT – Mjumbe;
e. Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, SMZ – Mjumbe;
f. Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – SMZ - Mjumbe;
g. Mkurugenzi wa Idara ya Muungano – SMT– Katibu/Katibu Mwenza; na
h. Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali– SMZ – Katibu/Katibu Mwenza.

Sekretarieti inaweza kushauri kualikwa kwa washiriki wengine inapoonekana inafaa.

### 6.2 Majukumu

Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja itakuwa na majukumu yafuatayo: -

a. Kuratibu vikao vya ngazi zote za Kamati ya Pamoja;
b. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya vikao na kuandaa taarifa;
c. Kutoa ushauri kwa ngazi zote za Kamati ya Pamoja;
d. Kutunza kumbukumbu za vikao vya ngazi zote; na
e. Kufanya kazi zote itakazopangiwa.

### 6.3 Uendeshaji wa Kikao

Kikao hiki kitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao: -

a. Kikao kitafanyika mara nne kwa mwaka na kutokana na mahitaji kikao maalum kinaweza kuitishwa;
b. Uamuzi wa kikao utafanywa na Mwenyekiti baada ya makubaliano ya Wajumbe wa Sekretarieti; na
c. Kikao kitafanyika pande zote mbili za Muungano kwa mzunguko. Hata hivyo, kinaweza kufanyika upande mmoja mfululizo kwa makubaliano.

## 7.0 VIKAO VYA SEKTA

Kutakuwa na vikao vya sekta ambavyo vitaitishwa na sekta zenye hoja au na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ. Lengo la vikao hivi ni sekta husika kuwa na uelewa wa pamoja juu ya hoja iliyopo na kuangalia namna bora ya kutafuta ufumbuzi na kushauri ipasavyo kwa ngazi zinazofuata.

## 7.1 Wajumbe

Wajumbe wa vikao hivi wanaweza kuwa wa ngazi yoyote katika sekta husika.

## 7.2 Uendeshaji wa Vikao vya Sekta

Vikao vya sekta vitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:-

a. Vikao hivi vitaitishwa wakati wowote kulingana na mahitaji na kwa kuzingatia maelekezo;
b. Sekta zitashauriana na Sekretarieti katika maandalizi na utaratibu wa uendeshaji wa vikao hivi; na
c. Sekta zitaandaa taarifa ya pamoja kwa ajili ya kuwasilisha kwenye ngazi husika.

## 7.3 Uwasilishaji wa Hoja

Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais zitapokea hoja zinazoleta changamoto katika utekelezaji wa masuala ya Muungano kutoka Wizara za Muungano na zisizo za Muungano. Kwa mantiki hii, hoja zinatakiwa kuwasilishwa mapema ili kutoa fursa ya kutosha kujadiliwa katika ngazi zote, ngazi ya sekta husika hadi katika kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ.

## 7.4 Uondoshwaji wa Hoja

Baada ya hoja kupatiwa ufumbuzi, kutaandaliwa maandishi ya uthibitisho wa kumalizika hoja hizo na kusainiwa na Mawaziri wa Sekta husika.

### 7.5 Gharama za Vikao

Kamati ya Pamoja inasimamiwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hufanya shughuli zake kupitia vikao katika ngazi tofauti. Vikao vya Kamati ya Pamoja katika ngazi zote vitagharamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Gharama hizo zitakuwa ni ukumbi, chakula na shajala.

## 8.0 TATHMINI NA UFUATILIAJI

Sekretarieti itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Pamoja ili kuhakikisha utekelezaji unafanyika ipasavyo. Baada ya kikao cha Kamati ya Pamoja, Wizara au Sekta zilizopewa maagizo zitatakiwa kutekeleza maagizo na maelekezo kwa wakati uliopangwa, kinyume na hapo watatakiwa kutoa taarifa ya changamoto zinazojitokeza ili maelekezo zaidi yatolewe. Aidha, Wizara zenye maagizo zinatakiwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maagizo hayo Ofisi ya Makamu wa Rais, SMT na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, SMZ katika kipindi kilichotolewa kwa ajili ya rejea.

## 9.0 HITIMISHO

Serikali zote mbili zina nia thabiti ya kuondosha mambo yote yanayoleta vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Kwa hiyo, ufanisi wa vikao hivi utasaidia kupunguza au kuondoa changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano hatimaye kuimarisha Muungano kwa manufaa ya pande mbili za Muungano. Pia, vikao hivi vinatoa fursa kwa Wizara, Idara na Taasisi za pande zote za Muungano kubadilishana uzoefu na jinsi ya kukabiliana na changamoto mbalimbali za maendeleo ya wananchi kwa ujumla.